**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU**

**6 APRILI, 2017**

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA TATU TAREHE 6 APRILI, 2017

### I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1 Ndugu Charles Mloka
2 Ndugu Neema Msangi
3 Ndugu Joshua Chamwela

### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

(i) Mhe. Jenista J. Mhagama (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu) aliwasilisha nakala za *Gazeti* la Serikali zifuatazo:-

- Toleo Na. 4 la tarehe 27.1.2017
- Toleo Na. 5 la tarehe 3.2.2017
- Toleo Na. 6 la tarehe 10.2.2017
- Toleo Na. 7 la tarehe 17.2.2017
- Toleo Na. 8 la tarehe 24.2.2017
- Toleo Na. 9 la tarehe 3.3.2017
- Toleo Na. 10 la tarehe 10.3.2017
- Toleo Na. 11 la tarehe 17.3.2017
- Toleo Na. 12 la tarehe 24.3.2017

(ii) Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2017/2018;

(iii) Mwakilishi wa Kamati ya Katiba na Sheria aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu na makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

(iv) Mhe. Josephat S. Kandege aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mfuko wa Bunge;

(v) Mhe. Kemilembe J. Lwota aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Uratibu na Udhibiti UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(vi) Mhe. Cecil D. Mwambe aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

## III. MASWALI

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 19: Mhe. Jerome D. Bwanausi

Nyongeza: Mhe. Jerome D. Bwanausi
Mhe. Yahaya O. Massare

### WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 20: Mhe. Sophia H. Mwakagenda

Nyongeza: Mhe. Sophia H. Mwakagenda
Mhe. Naghenjwa L. Kaboyoka
Mhe. Mendrad L. Kigola

Swali Na. 21: Mhe. Jasson S. Rweikiza

Nyongeza: Mhe. Mhe. Jasson S. Rweikiza
Mhe. Savelina S. Mwijage
Mhe. Alex R. Gashaza

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 22: Mhe. Jaku H. Ayoub

Nyongeza: Mhe. Jaku H. Ayoub
Mhe. Maryam S. Msabaha
Mhe. Ally M. Keissy

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 23: Mhe. Magdalena H. Sakaya

Nyongeza: Mhe. Mhe. Magdalena H. Sakaya
Mhe. Shally J. Raymond
Mhe. Pauline P. Gekul

**MATANGAZO:**

i. Wageni mbalimbali waliokuwa Ukumbini walitambulishwa
ii. Saa 7.00 mchana kutakuwa na Ibada ya CCT itakayoongozwa na Mwalimu Mwakasege katika Ukumbi wa Basemate.
iii. Mhe. Aida J. Khenan alitangazwa amepata ajali ya pikipiki.

**MWONGOZO WA SPIKA:**

Wabunge wafuatao waliomba Mwongozo:-

(i) Mhe. Joseph O. Mbilinyi - aliomba mwongozo na kueleza kuhusu tukio la watu wenye silaha kuvamia Studio ya Muziki na kuteka wasanii jana jijini D'Salaam. Je, matukio hayo yanachochewa na nani?

Spika – Serikali imesikia na itafanyia kazi suala hilo.

(ii) Mhe. Frank G. Mwakajoka – aliuliza juu ya Faru Felister kutumia fedha nyingi kiasi cha Sh. 64 milioni kwa mwezi. Je, fedha hizo haziwezi kuokolewa;

Spika – Serikali italifanyia kazi.

(iii) Mhe. Mwita M. Waitara – aliomba mwongozo kuhusiana na suala la njaa na kupanda kwa bei za vyakula;

(iv) Mhe. Alphaxard K. Lugola – aliomba mwongozo kuhusiana na video inayosambaa mitandaoni ikionyesha Kiongozi wa Upinzani Bungeni akitukana Bunge na Chama cha Mapinduzi kuhusiana na uchaguzi wa EALA;

Spika aliahidi kuchukua hatua kali za kinidhamu.

(v) Mhe. Joseph K. Mhagama aliongezea kuhusu kitendo cha Kiongozi wa Upinzani kudharau Bunge na Serikali.

**UAMUZI WA SPIKA**

Kuhusiana na vitendo vya vurugu na maneno ya Wabunge kwenye uchaguzi wa EALA Spika alitoa maamuzi yafuatayo:-

(i) Mhe. Halima J. Mdee ambaye alitoa maneno ya matusi kwa Spika apelekwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge mara moja;

(ii) Mhe. Freeman A. Mbowe (KUB) afikishwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge mara moja.

Aidha, Spika aliagiza Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhe. Alexander Pastory Mnyeti naye afike mara moja kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili ahojiwe kuhusu tuhuma za kulidhalilisha Bunge.

## IV. HOJA ZA SERIKALI

- Waziri Mkuu alisoma Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yake na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kutoa Hoja ya kuliomba Bunge likubali kupitisha Bajeti hiyo.

- Mhe. Joseph K. Mhagama, alisoma Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

- Mhe. Hawa A. Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alisoma Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji, makadirio ya mapato na matumzi ya Ofisi ya Bunge.

- Mhe. Dkt Hadji H. Mponda, alisoma Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji, makadirio ya mapato na matumizi ya Tume ya uratibu na udhibiti wa UKIMWI.

**TANGAZO:**

Kesho Ijumaa tarehe 7.4.2017 kutakuwa na Semina kuhusu Rushwa itakayotolewa na APNAC, katika Ukumbi wa *African Dreams Hotel*.

Ibada ya Mchungaji Mwakasege itafanyika leo saa 7:00mchana.

## V. KUSITISHA BUNGE

Saa 10:00 jioni Bunge lilisitishwa hadi saa 10:00 jioni.

## VI. BUNGE KURUDIA

Saa 10:00 jioni Bunge lilirudia, Hoja ya Waziri Mkuu iliendelea.

Mhe. Freeman A. Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni alisoma maoni ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

## MWONGOZO

Mhe. Jenista J. Mhagama aliomba mwongozo na kutaka Msemaji wa Upinzani aondoe maneno kwenye Hotuba yake yanaingilia uhuru wa Mahakama na kuzungumzia mwenendo wa Rais.

Baada ya kulumbana kwa muda, maneno hayo yaliondolewa na msemaji wa Kambi ya Upinzani aliendelea kusoma Taarifa yake.

Uchangiaji wa jumla ulianza kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jarome Dismass Bwanausi - CCM
2. Mhe. Edward Franz Mwalongo - CCM
3. Mhe. Godbless Jonathan Lema - CHADEMA
4. Mhe. Masoud Abdallah Salum - CCM
5. Mhe. Amina Saleh Mollel - CCM
6. Mhe. Dkt. Diodorus Buberwa Kamala - CCM
7. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby - CCM
8. Mhe. Stephen Julius Masele - CCM
9. Mhe. Kunti Yussuf Majala - CHADEMA
10. Mhe. Godfrey William Mgimwa - CCM
11. Mhe. Janeth Zebedayo Mbene - CCM
12. Mhe. Sebastian Simon Kapufi - CCM
13. Mhe. Maryam Salum Msabaha - CHADEMA
14. Mhe. Hussein Mohammed Bashe - CCM
15. Mhe. Anna Richard Lupembe - CCM
16. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka - CUF
17. Mhe. Joseph George Kakunda - CCM

## VII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 1.45 usiku Mhe. Spika aliahirisha Bunge hadi Jumatatu tarehe 10 Aprili, 2017.